**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY (TPHPA)**

TPHPA
TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA (TPHPA) YATUNUKIWA CHETI NA SHIRIKA LA FORODHA DUNIANI

26 Januari, 2026 Arusha.

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) inautaarifu umma kuwa imetunukiwa cheti cha kutambua mchango wake katika kuimarisha usalama wa mipakani na udhibiti wa bidhaa kutoka Shirika la Forodha Duniani (World Customs Organization – WCO).

Cheti hicho kimetolewa katika hafla iliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), iliyofanyika tarehe 26 Januari, 2026 katika Ukumbi wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam. Hafla hiyo ilihusisha taasisi za Serikali na wadau wengine wa sekta ya forodha na udhibiti wa mipakani.

Kutunukiwa kwa cheti hicho kunatokana na utekelezaji wa majukumu ya TPHPA katika kulinda afya ya binadamu, mimea na mazingira dhidi ya athari zitokanazo na matumizi yasiyo salama ya viuatilifu. Majukumu hayo yanajumuisha udhibiti wa uingizaji, usambazaji na matumizi ya viuatilifu nchini kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Aidha, TPHPA imeendelea kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na taasisi nyingine za Serikali katika kuimarisha usalama wa mipakani na kuwezesha biashara halali.

TPHPA inaeleza kuwa kutambuliwa huku ni matokeo ya juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha mifumo ya udhibiti wa bidhaa, kulinda afya ya jamii na mazingira, pamoja na kuwezesha biashara salama na endelevu.

Mamlaka inatoa shukrani kwa Shirika la Forodha Duniani (WCO), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wadau wote kwa ushirikiano unaoendelea, na itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi kwa maslahi ya Taifa.

**Imetolewa na:**
Kitengo cha Uhusiano wa Umma na Mawasiliano
Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA)

TANZANIA PLANT HEALTH AND
PESTICIDES AUTHORITY
P.O. Box 3024, Tel.: +255 27 297 0487
ARUSHA - TANZANIA